“Yesu Kristo ni Yeye Yule, jana na leo na hata milele“
(Ebr. 13:8)

Baruwa ya Mzungoko **Mwisho wa mwaka 2018**

Myaka Mingi katika Kazi ya BWANA wangu katika Miji yakaribu na Inchi za Mbali

Somo la Muhimu:
Ujumbe wa Mwisho mbele ya Kurudi kwa Kristo

Kwa moyo wangu wote nina wasalimu wandugu na wa dada ulimwenguni pote katika Jina tukufu la BWANA wetu Yesu Kristo na andiko kutoka 1. Thes 3:13:

> ***“Apate kuifanya imara mioyo yenu iwe bila lawama katika utakatifu mbele za Mungu, Baba yetu, wakati wa kuja kwake BWANA wetu Yesu pamoja na watakatifu wake wote!“***

Hapo kwa sura ifuatayo ya shahiri 13 hadi 17, Mtume aliionyesha namna itakavyo tendeka wakati wa kurudi kwake. *“…kwa kuwa twa waambieni haya kwa* ***Neno la BWANA,*** *kwamba sisi tulio hai, tutakao salia hata wakati wakuja kwake BWANA, hakika hatuta watangulia wao walio kwisha kulala mauti.*

Kwa sababu ***BWANA mwenyewe atashuka kutoka mbinguni*** *pamoja na* ***mwaliko,*** *na* ***sauti ya malaika mkuu****, na* ***parapanda ya Mungu; nao walio kufa katika Kristo wata fufuliwa kwanza;*** *Kiisha sisi tulio hai, tulio salia,* ***tutanya kuliwa pamoja nao katika mawingu,*** *ili tumulaki BWANA hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na BWANA milele“* (1. Thes. 4:15-17). Mwaliko, sauti, na sauti ya tarumbeta itasikilika wakati wa ufufuko, kubadilishwa na kunyakuliwa.

Sasa kwa mwisho wa wakati wa neema, kelele ya usiku wa manane ina sikilikana kuita waamini wote***: „Naye, BWANA-***

arusi: anakuja, tokeni mwende kumlaki“ (Mt 25). Ujumbe halisi wa Neno unatangulia Kuja kwa Pili kwa Kristo.

Ujumbe wa mwisho ulichukuliwa tangu myaka mingi. Lakini Kuja kwake kutakuwa kwa gafla, kulingana na yale BWANA mwenyewe alisema*: „Kwa maana kama vile umeme utokavyo mashariki ukaonekana hata magharibi,* ***hivyo ndivyo kutakavyo kuwa kuja kwake kwa Mwana wa Adamu“*** **(**Mt 24:27). Hiyo itafanyika kama vile kufumba na kufumbua*:* ***„...kufumba na kufumbua wakati*** *wa parapanda ya mwisho;* ***...na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika“*** **(**1 Kor. 15:52).

Paulo ameeleza sana kwenye baruwa nyingi akionyesha namna gani mambo haya yatatendeka na vitu gani vitakavyo fanyika kwa wakati huo. Mitume wote walieleza kuhusu kuja kwa Pili kwa Kristo katika Baruwa zao. 1. Thes 5:23 mutume alimaliza akisema maratena kuhusu somo hiyo: ***„Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; ninyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe muwe kamili, bila lawama watika wa kuja kwa BWANA wetu Yesu Kristo!“***

Kwa wakati mtu wa Mungu Willliam Branham alisema mara 1, 400 matayarisho ya bibiarusi wa Kristo kwa ajili ya unyakuo. Alifanya hivyo akiwa chini ya utume wa BWANA. Kupitia hudma ya kipekee **yote yangelipashwa kwanza kurudishwa na kuwekwa kwa nafasi yake katika Kanisa. Hii ndiyo ahadi ya wakati wetu:** ***„Naye akajibu, akawaambia, kweli Eliya yu aja kwanza, naye atatengeneza yote“*** (Mt 17:11; Mk 9:12).

Wakati ya muhimu kwa mwisho wa wakati wa neema imekuwa sehemu ya utangazaji wangu kwa myaka mingi kupitia hudma yangu, pamoja na mafundisho yote ya kibiblia. Niliacha kila somo kwa hali ya kulingana na ginsi inavyo andikwa katika Biblia. Nimetupilia mbali kila matafsiri. Wakati umepita; ahadi ya kurudi (Jn 14) kwa BWANA na mkombozi ni karibu sana mkononi. Nikuhusu ujao wa kurudishwa wa musingi ya kibiblia kama vile matayarisho ndani ya imani na kutii kwa ajili ya siku ya utukufu wa Kristo (Flp 1:6).

Paulo, alie tangaza Neno kwa utume wa Kimungu aliwaamusha wa filipi na maneno haya ***„...Mkishika neno la uzima;***

nipate sababu ya ku furahi katika ***siku ya Kristo,*** *ya kuwa sikupiga mbio bure wala siku jitaabisha bure.“* (Flp 2:16). Hivyo ndivyo nami ninavyo amsha sasa waamini wote wa Biblia, katika mataifa yote na lugha zote, kupitia utume wa kimungu.

Katika ufunuo 19:7; kundi la watu wengi walio nyakuliwa kutoka duniani wana imba***: „Natufurahi, tukashsngilie tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya mwana kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari…“*** Katika Mt 25:10 imeandikwa: ***„…Nao waliokuwa tayari, wakaingia naye arusini; mlango ukafungwa.”***

Tunaishi kwa wakati wa muhimu sana mbele ya kurudi kwa Kristo; hapo sasa inastahi semeka na kusemeka mara tena, ili waamini wote wa kiblia walisikie na kuliamini: Tarehe Juni, 11, 1933, kuna kitu cha ajabu kilicho tendeka: wakati muhubiri kijana William Branham alipo kuwa akibatiza waamini katika mto Ohio, kishindo lilitoka mbinguni na wingu kubwa la kimaajabu lenye nuru lilishuka, wazi wazi machoni pa watu wote walioku wa mahali pale. Hapo sauti lenye nguvu lili sikilika**: “Kama vile Yohana mbatizaji alivyo tumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, Umetumwa na ujumbe ambao utatangulia kuja kwa pili kwa Kristo“.** Ndugu Branham alilinganisha hii tukio hili la kimaajabu, katika mahubiri mengi tofauti mara 18. Aliweka mkazo kwa mba**: “Si mimi mutangulizi, baali Ujumbe ndiyo utakao tangulia“.**

Utume halisi na masomo nyingine ziligeuzwa na wale waabudu Branham huko Marekani, walipo andika yafwatayo*: „Kama vile Yohana Mbatizaji alivyo tumwa kutangulia kuja kwa kwanza kwa Kristo, nawe unatumwa kutangulia kuja kwake kwa pili“.*

Mtu alietumwa kutoka kwa Mungu alitangaza mafundisho yote ya kibiblia; kwa kweli alitangaza shahuri zote za Mungu ili kila kitu katika Kanisa la Yesu Kristo kirudi kwanafasi yake kamili. Ali sisitiza ya kwamba Mungu moja wa milele alijifunua yeye mwenyewe kwa ajili ya okovu wetu, kama vile Baba mbinguni katika Mwana wake mpendwa hapa duniani na kupitia Roho mtakatifu katika Kanisa lake. Mungu alikuwa katika Kristo akiuambatanisha ulimwengu pamoja naye (2. Kor 5:19, 1. Tim 3:16).

Ndugu Branham alihubiri Injili kwa Ujao, kama vile Petro na Paulo walivyo fanya kwa wakati wao. Alielewa vizuri kazi yake kubwa ya utume katika Mt 28:19 Ilikuwa ina husu *Jina* ya ubatizo, na moja Marko 16:16, mahali inayo husika na Imani, na katika Luka 24:47 mahali munapo semeka kuhusu usamaha wa dhambi. Ali hubiri msamaha wa dhambi kupitia damu ya Kristo iliyo tolewa, na alibatiza waamini kama vile Petro alivyo iagiza kwa mahubiri yake ya kwanza siku ya Pentecoste, kupitia chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. *"Tubuni, na mukabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi…"*

Siku hiyo nafsi Elfu tatu ziliamini kupitia mahubiri yake ya kwanza chini ya umwangaji wa Roho mtakatifu, na walibatizwa (Matendo 2:14-41).

Katika Kanisa la kwanza wale wote walio amini, kati ya wayuda, wa samaria ao mataifa walibatizwa katika Jina la BWANA Yesu Kristo (Matendo 8:16; Matendo 10:48). Wanafunzi wa Yohana Mbatizaji nao walibatizwa namna hiyo „*Walipo sikia hayo,* ***walibatizwa katika Jina la BWANA Yesu"*** (Matendo 19:5). Ubatizo katika majina matatu ao chochote kama kile hakija kuweko katika Biblia, ilianzishwa na Athanase kwa karne ya nne.

Vipindi vya wakati maalum

Kwa Disemba, 24, 1965 kipindi cha Baraka kilifikia mwisho. BWANA Mungu alimchukuwa kwake mtumishi na Nabii wake. Nilihuzuria mazishi yake kwa huzuni, ambao ilifanyika siku ya Jumatatu ya pasaka, Aprili, 11, 1966. Nafsi ilijaa huzuni. Wakati machozi na huzuni nyingi vilinijaa. Sauti ilisema maranyingi nami moyoni wangu: „Sasa wakati wako una kuja wa kwenda muji kwa muji kulihubiri Neno na kugawa chakula cha Kiroho". Hapo nilijua kwamba wakati wangu umefika.

Kwa Aprili, 1966 kipindi kipya kilianza: ama kwa masemi mengine mwendeleo. Lakini, hayo yaliwezekana je? Utume wa BWANA mwenyewe, hapo baada ya mazishi, siku ya Aprili, 12 na 13, 1966, niliwa kusanya wandugu wote pamoja huko Jeffersonville. Lengo langu lili kuwa ya mahubiri yote yaliyo wekwa kwenye kanda yaweze kutafsiriwa kwa lugha nyingi tofauti. Roy

Borders aliyekuwa mwandishi wa kipekee wa ndugu Branham ambaye nilie mjuwa, aliwekwa kwa ajili ya ku angalilia chumba cha unchapaji. Hivyo ndivyo ilivyo anza "Utangazaji wa Neno lililonenwa"{Spoken word Publication}.

Ikiwa BWANA mwaminifu a singeli mpata mtumishi wake William Branham huko Jeffersonville siku, Juni, 1933, Hatungeliweza kusikia kitu kuhusu Ujumbe. Ikiwa BWANA mwaminifu a singeli mpata mutumishi wake Ewald Frank huko Jeffersonville kwa Aprili, 1966, ulimwengu hungewaza kusikia kwamba kuna Ujumbe.

Kwa 1973, nili safiri kwenda Jeffersonville nikisindikizwa na mwongozi wetu wa kanisa na mzee, Ndugu Leonhard Russ na Ndugu Erich Schwill. Wandugu wa hapo walituonyesha mahali Ndugu Branham alibatizia kwenye mto Ohio wakati mambo ya kimaajabu yalite ndeka. Pia tuli tembea kuona maskani ya ndugu Branham na majengo ya "Spoken Word" (Neno lililonenwa).

Yusufu, mtoto wamwisho wa Ndugu Branham alikuwa karibu na myaka 11 kwa Aprili, 1966. Kwa 1980, aliyiita jina tena kutoka "Spoken Word Publication" (Utangazaji wa Neno lililonenwa) kuwa "Voice of God Inc." (Sauti ya Mungu) wakati huo nili kuwa nimekwisha tembea karibu nusu ya dunia ni kiuchukua Ujumbe wa Neno. Mbele ya kufanya kazi ya utume wa Kimungu, inaomba kwanza mwito wa kimutume na kutumwa kwa hapo hapo utangazwe.

Na sema hii mbele ya BWANA Mungu: Wakati sauti ya baragumu ya Malaika wasaba wa Ufun 10:7 ilipotangazwa kama vile: „Sauti ya Mungu" maabudu ya Nabii ilianza. Ufun 10:7 haisemi lolote kuhusu sauti ya Mungu. Katika Ufun 8 na 9, Inaonyesha wale Malaika wa sita wa baragumu ambao wataleta hukumu zao juu ya dunia. Katika ufun 10:7 tunakuta *tangazo* la yale ambayo yata kao timia wakati Malaika wa saba atakapo piga Baragumu: Hapo ndipo **Siri ya Mungu** itatimilika kama vile alivyo waambia watumishi wake manabii.

Katika ufun 11, nyuma ya wale washuhuda wawili kumaliza kazi zao na Hekalu lilipokwisha jengwa na kupimwa: „*Malaika wa saba anapiga Baragumu* (kama vile ginsi ilivyo tangazwa katika ufun 10:7). *Paka wa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, ufalme*

wa dunia umekwisha kuwa wa BWANA wetu na wa Kristo wake; naye atamiliki hata milele na milele" (Ufun 11:15). Amina.

Mambo yote ambao wanaelekeza kuhusu Ufun 6 na kwa sura zingine munamo pia yatakayo kuja. Ndugu Branham alisema yale yote yaliyo tajwa katika muhuri wa sita na muhuri wa saba yote inaelekea kuhusu dhiki kubwa. Ufun 10 inaonyesha yale yatakayo tendeka wakati BWANA, kama Malaika wa Agano, ana weka miguu yake kwenye Nchi na Juu ya Bahari. Ila tu *"Wakati* (na si kwa mwaka hii 1963) *hata ngurumo saba zilipotoa sautiya zo… na Yule malaika akainua mkono wake wa kuume kuekea mbinguni akaapa…"* (shahiri 4-6). Kulingana na Dan 12:7, kunabaki tena myaka 3 kusema ifike mwisho wa hiyo wakati. **Ufun 10:7, inabaki na itaendelea kuwa kwa umoja. Ndugu Branham alisema kila mara kuhusu masiri za Mungu. Paulo naye alifanya hivyo*: „Mtu na atuhesabu hivi, kuwa tu watumishi wa Kristo, na mawakili wa siri za Mungu"*** (1. Kor. 4:1).

Siri ya Mungu; ni Yesu Kristo BWANA wetu. Mtume aliweka mkazo mara moja tena*: „…ili wafarijiwe mioyo yao, wakiunganishwa katika upendo,* ***wapate kujua kabisa siri ya Mungu, yaani Kristo; ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifu zime sitirika"*** (Kol 2:2-3).

Kwa Februali, 1980 huko Marseille, Nili ulizwa swali kuhusu ngurumo saba mara ya kwanza. Hapo sikujibu chochote lakini asubui iliyo fuata, BWANA akaniita na sauti yenye nguvu. **"Mutumishi wangu, amka na ukasome 2. Tim 4."** Mtu hawezi kujiuliza namna gani ninavyo jisikia wakati kama huo. **Hapo BWANA mwaminifu aliniambia maneno haya kwa kipekee.** Ndipo nilipo kuwa niki soma*:* ***„Lihubiri neno, uwe tayari, wakati unao kufaa na wakati usiokufaa, karipia, kemea kuonya kwa uvumilivu wote na ma fundisho"***. (shahiri 2). Nilitambua vema kwamba hakuna kitu kilicho andikwa kuhusu ngurumo saba; hapo nikusema hakuna kitu chochote kinacho stahili kuhubiriwa kuhusu hiyo.

Kazi yangu inahusika na kuhubiri. Neno lililo andikwa tu. Kwenye mishahiri matatu ya kwanza katika Ufunuo sura 1, tunasoma. ***„Heri asomae na wao waya sikiao maneno ya unabii huu, na kuyashika yaliyo andikwa humo, kwa maana***

wakati ukaribu“ (Shahiri 3). Ndugu Branham alilinganisha mishahiri mine katika Ufun 22 mara 150. Mtu yeyote atakae ongeza wala kupunguza kitu chochote kwa haya yaliyo andikwa, kwa sehemu ya mti wa Uzima**: „Usikubali chochote kama hakiandikiwe katika Biblia“.**

Kila mhubiri ange weza kusoma kwa makini 2Tim 4 na kujipima, ili aone kwamba shahiri ya 2 kama ana hubiri Neno pekee. Ao shahiri la 3 na la 4 kama zina muhusu, ao kama anahubiri hadidhi za wanadamu. Yeyote asiye heshimu kila Neno la Mungu ana hukuniwa kwa kuamini matafsiri yao binafsi na mafundisho ya uongo (2. Thes 2:10-12).

Mimi simu kosowi Nabii, ila ni uajbu wangu wa kuweka kila kitu kwa nafasi yake katika maandiko kulingaana na utaratibu ya Kimungu. Kuhusu yale yote aliyo yasema yanayo lingingana na mpango wa okovu wa Mungu. Ni napashwa ku waambia wale wote wanao jilinganisha naye na kwenye Nukuu zake, yale ambao Petro aliyo yasema akilinganisha mabaruwa za Paulo***: „Vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyraka hizo yamo mambo, ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasiyo na elimu, wasiyo Imara, huyapotoa, kama way a potoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe“*** (2Pet 3:16).

Ndugu Branham alikuwa akiongea mara nyingi kuhusu mambo yatakayo kuja, anayaeleza kama vile mambo iliyo pita. Lakini hivi ndivyo ilivyo hata kwa unabii zote za kibiblia. Kwenye kisanga cha patimo, Yohana aliona mambo yote kuwa ya litendeka; Isipo kuwa tu wale wajinga wakiroho, wao ndio wenye wanao geuza ma nukuu kwaajili ya maangamizi ya kiroho kwa wale wanao wa sikiliza.

BWANA wetu alimshuhudia Yohana mbatizaji kwamba alikuwa mkuu kiliko nabii, lakini haja kuwa mkuu kuliko mtu.“Lakini kwa nini mlitoka? ni kuona nabii? naam, nawaambia, na alie mkuu zaidi ya nabii“. Na hapo BWANA wetu aliweka mkazo: “*Huyo ndie alie andikiwa haya,* ***tazama, mimi namtuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, atakae itangeneza njia yako mbele yako“*** **(**Mt 11:9+10). Neno lile linabaki ukweli kama neno ya Ndugu William Branham. Mitume wote walitangaza kurudi kwa

BWANA lakini William Branham alipewa kazi ya hapo hapo, ya kuleta ujumbe unao tangulia kuja kwa pili kwa Kristo.

Alikuwa mwanadamu kwa namna yoyote, mtu alie tumwa na Mungu. Lakini karama ya kimungu ya kufunuliwa na hudma ya kinabii ya Ndugu Branham, haingeliweza kushindwa na ilikuwa kamili. Kama mwanadamu naye pia alikuwa na maoni ya mambo, kwa mufano, alikuwa amekubalishwa ya kwamba maono aliyoyaonyeshwa kwa mwaka wa 1933, kuwa ita itatimilika kwa mwaka 1977; Washabiki wandugu Branham walifundisha kwamba kila kitu kita kwisha kwa mwaka wa 1977 na kwamba unyakuo utakuwa umefanyika. Lakini inabaki kuwa kweli milele ya kwamba hakuna mtu anaye jua siku wala saa.

Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazita fautikani!

Kwa utukufu wa Mungu, nina weza kushuhudia yale niliyo pewa kwa neema yake. Kwa myaka 70 iliopita niliishi mazoezi yangu na kutakasiya BWANA maisha yangu. Ni baada ya vita ya pili ya dunia nilipo mkubali Yesu Kristo kama mkombozi wangu binafsi, wakati ya mukutano wakwanza ya utangazaji wa injili chini ya hema iliyo fanyika kwa Juni, 1948. Karibu ya Juni, 14, 1948, ndipo David Ben-Gurion alitangaza kuanza kwa Ichi ya Israeli.

Kwa Juni, 1949, wakati wa mikutano ya ajabu ya kipentecosti huko Hambourg, ndipo nilipo pokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kwa Ogusti 1955 huko Karlsuhe, ni lihuzuria mara ya kwanza mukutano wa ndugu Branham na sikuya jumatatu, 15, 1955, nili mkuta nikiwa pekeyangu mara ya kwanza. Siku Juni, 12, 1958 huko Dallas huko Taxas, nilipata mudawakuongea naye maongezi ya kutosha. Siku, Aprili, 2, 1962 nilipata mwito wa hudma yangu kwa namna ya mazoezi ya yangu. Kwa kweli tangu wakati ule naweza kusema, „Maisha yangu yamekuwa katika kazi ya BWANA wangu, kwenye miji ya karibu hata na kwa inchi za mbali.“

Nime kwisha toa ushuhuda wa mazoezi yangu yenye nguvu nyingi mara ya siku Aprili, 2, 1962. Ninataka niseme tena kuhusu vitendo vilivyo tendeka kwa mwaka 1962. Kupita simu nilitayarisha mazungumuzo ya kipekee pamoja na ndugu Branham huko Jeffersonville kwe mwanzo ya mwezi wa Disemba. Siku ya Jumapili, 2, Disemba nilikaa pamoja na waabudu kwenye maskani ya ndugu Branham. Hapo mchungaji ndugu Neville, aliomba makutano wasimame kwa ajili ya maombi, Ndugu Heckerson ali paaza sauti kubwa: „Asema BWANA Mungu: Mwanangu Frank, haukuvuka bahari kubwa kwa bure. Usikate tumaini kwa sababu hukumkuta nabiiwangu siku ya jana, utakutana naye siku ya kesho, naye atakueleza yote yaliyo moyoni mwako".

Mchungaji Neville aliniita katika mikutano miwili nilio shiriki kuwa na Neno mbele ya kusanyiko. Nilikuwa na heri ya kuhubiri mara mbili kwenye madhabahu ambapo nabii alihubiria mahubiri yake.

Ilitimia kama vile Ndugu Hickerson alivyo isema katika unabii: Ndugu Branham alinitoa kwenye Hotel siku ya Jumatatu, na tuliongea kwamuda mrefu. Mbele ya wandugu wawili, Fred Sothman na Banks wood, nabii alirudilia maneno ambao BWANA alikuwa ameniambia siku, Aprili, 2, 1962. Aliniambia kwamba njaa haiku linganishwa na chakule cha mwili, kama vile nilivyo wazia baali ilikuwa ni chakula cha Kiroho ambacho ningeweza kugawa. Ndugu Branham alishushuhudia mwito wangu kupitia ufunuo na alijibu maswali yaliyo kuwe moto katika moyo wangu. Kwa kumaliza, alisema**: „Ndugu Frank subiri kwa ugawiji wa chakula mpaka utakapo pata mabaki yake".** Mabaki yana kutwa katika mahubiri Kuhusu mihuri saba ya machi, 1963 mpaka kwa mahubiri ya mutu wa Mungu kwa Disemba, 1965, ambao ilitumwa kwangu. Ni kwa wakati huo ugawaji wa chakula ungelianza.

Ugawaji wa chakula cha kiroho unastahili kuwemo na utangazaji wa Neno lililo andikwa: *„Angalia, sikuinakuja, asema BWANA Mungu, ambazo nitaleta njaa katika Nchi; si njaa ya kukosa chakula, wala kiu ya kukosa maji, baali* ***ya kukosa kuyasikia maneno ya BWANA…"*** (Amos 8:11) BWANA alisema:

„Imeandikwa, ***mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.“*** (Mt 4:4)

Mwito ya hudma niya muhimu kwangu kama vile BWANA alivyo ongea na Ibrahimu katika mwanzo 12 na Musa katika kutoka 3 na Yoshua katika sura ya kwanza ao kama vile ilivyo kuwa hata kwa Yohana mbatizaji katika Luka 3, na kwa Paulo katika Matendo 9 na kwa Ndugu Branham siku Juni, 11, 1933 na siku Mai, 7, 1946. Kila kuitwa na kutumwa kwa Kimungu kulikuwa kukia mbatanishwa na mpango wa Okuvu wa Mungu***: „Kweli, kweli na waambieni: anayempokea mtu Yule ni nayemtuma, anipokea; naye anaye nipokea mimi, anampokea Yule aliye nituma.“*** (Yn 13:20)

Tena ikafika siku ya Jumapili, Septemba, 1976, wakati BWANA mwaminifu aliiweka utume aliyo nipa katika maandiko**: „Mutumishi wangu, nimekuweka kulingana na Mt 24:45-47 kwa ugawaji wachakula kwa wakati unao faa“.**

Ndugu Branham aliona katika ono ginsi alivyo weka chakula tofauti kwenye rafu. Aliongea kuhusu hiyo siku Aprili, 1, na siku Disemba, 30, 1962. Nimepewa utume Wa Kimungu wa kutayarisha vema chakula kilicho wekwa na kukiweka kwenye meza ya BWANA kwa ajili ya taifa la Mungu. Na wandugu wote duniani pote wana gawa chakula kile kile cha kiroho, wakati wanapo hubiri Neno lililo funuliwa.

Mbinu za shetani za kale

Ni vigumu kwetu kuelewa namna gani iliwezakana kwa nyota ya Arfajiri, Mwana wa asubui, aweze kuinuka mbinguni. Aliitaji aweke kiti cha ufalme juu ya nyota za Mungu na ajifananishe na Yule alie juu zaidi (Isa 14 kutoka shahiri 12). Kwa sababu ya itaji yake ya kujiinua juu, kwa kusema: „Nataka…, nataka…“ na alikuwa msima mizi wa anguko lake, na hatima, na amekuwa adui mkubwa wa Mungu na adui waamini wote. Alichukuwa Malaika wote walio mufuata. Katika Ufun 12:7-9 inatwambia kama vita ya mwisho itapatikana mbinguni: ***„Na kulikuwa vita mbinguni;*** *Mikaeli na malaika zake wakapigana nayule joka, Yule joka akapigana nao pamoja na malaika wake, wala mahali*

pao hapa kuonekana tena mbinguni. Yule joka akatupwa, Yule mkumbwa, nyoka wa zamani, aitawaye ibilisi na shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye"



Kazi ya Kwanza ya kubatiza ya Ndugu Branham katika Mto Ohio siku Juni, 11, 1933.

Myaka 40 imepita nilipo sindikizwa na Ndagu Russ na Ndugu Schwill, nilitembelea mahali ambapo BWANA alishuka katika wingu kuu lenye nuru la kimaajabu siku Juni, 11, 1933. Alipo kuwa akimtuma ndugu Branham.

Huko Jeffersonville tuli enda kuona"Spoken word Publication“ (Utangazaji wa Neno Lililonenwa).

Iliyo jengwa na pangiliwa na Ndugu Roy Borders. Alikuwa mwandishi wa kipekee wandugu Branham hadi mwisho. (Kutoka mkonowa kushoto: Ndugu Frank, Borders, Russ, Schwill)

Kwa disemba 1962, nili kubaliwa kuhubiri mara mbili kwenye Madhabahu katika maskani la Ndugu Branham huko Jeffersonville, mahali Ndugu Branham alihubiria mahubiri yake ya muhimu.





Ndugu Branham na Yusufu, kijana wake mdogo, muda kidogo mbele ya kifo chake.

Kwa mwaka 1980 Yusufu, ali kamata uongozi wa“ Spoken Word Publications“ (Utangazaji wa Neno Lililo Nenwa) akaita jina tena la “Voice of God Recordings, inc“ (Sauti ya Mungu iliyo wekwa kwenye kanda).

Biblia ya Ndugu Branham Jinsi ailivyo iacha kwa 1965.

David Ben-Gurion akisema, utangazaji uhuru wa inchi ya Israeli.

"Maana BWANA atamuhurumia Yakobo, atamchagua Israeli tena, naye ata waweka katika nchi yao wenyewe ;atajiunga nao, nao wataambatana na nyumba ya Yakobo." (Isa 14:1)

"Alie mtawanya Israeli atamukusanya, na kumulinda, kama Mchungaji alindavyo kundi lake." (Yer. 31:10)

"Basi neno, BWANA Mungu asema hivi; nitawa kusanya ninyi toka kati ya kabila za watu, na kuwakutanisha toka nchi zile mlizo tawa nyika, nami nitawapeni nchi ya Israeli" (Eze 11:17)

"Na BWANA atairithi YUDA iwe sehemu yake katika nchi takatifu, naye atachaguwa Yerusalem tena." (Ezek 2:12)

"Basi kwa mtini jifunzeni mfano (Hos 9:10)***;Tawi lake likiisha ku chipuka na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno ni karibu..."*** (Mt 24:32)

Si vyepesi kwetu kuelewa kwamba baada ya kujiinuwa kwa shetani huko mbinguni na kuwa adui wa Mungu, aliendelesha mpango wake hapa duniani na kuleta anguko kwa mwanadamu hapo shambani mwa Edeni. Ndugu Branham alilionge lea zaidi, na hatapia kwa muhuri wa saba. Nani anaye weza kuelewa kwamba BWANA Mungu, alie kuwa akitembea. Katika Bustani ya Edeni, ali mruhusu shetani, joka la kale, kuwa na maongezi pamoja na Hawa na kupanda ndani yake mbegu ya mashaka yaneno la Mungu: **„Kwa kweli Mungu alisema…?“**

Wakati Hawa alitegea sikio kwake, hapo ndipo shetani aliweza kupanda ndani mwake mbegu ya shaka kuhusu yale Mungu aliyo kuwa ame mwambia Adamu, maovu yalitendeka. Hivyo ndivyo shetani alipata ushindi juu ya neno, kama vile ndugu Branham alivyo weka mkazo. Alizidi kusema kwamba: kutoamini ndiyo dhambi ya asili ambayo ina leta maasi yote. Yeye asie amini yale ambayo BWANA Mungu alisema amehukumiwa kuamini uongo wa shatani.

Ndugu Branham alitaka ahubiri kuhusu „kondo la nyoka”siku Disemba, 24, 1965, na alikuwa amekwisha tayarisha mahubiri kuhusu hayo na kwa siku hiyo akaitwa nyumbani. Kwa mwanzo nyoka alitumia hila na ujanja, na kwa mwisho nyoka anafanya sawa sawa kama vile kwa Hawa ilitokana na mapenzi ya Mungu yasiyo makamilifu, ili mpango wa Mungu wa ukombozi upate kutendeka katika mpapenzi ya Mungu makamilifu. Kwa upotevu wake ali mleta Adamu chini ya ushawishi wake, ikamuweka vile vile katika anguko la dhambi. Mbegu mbili tofauti zilionekana ku kaini na Abeli; hapo uadui ulianza. Hiyo ndiyo iliyo kuwa njia ya Mungu ya kuanzisha mpango wake wa Okovu. **Baada yahayo, BWANA Mungu ndipo alitoa ahadi ya kwamba uzao wa Mungu utatokea kwa mwanamke na utavunja kichwa cha nyoka** (Mwanzo 3:15). **Na baadae lawama ilitajwa kwa Adamu: *„Kwa kuwa umeiskiliza sauti ya mke wako…!“*** (Shahiri 17).

Huzuni ni kwa mwisho ya myaka 70 shetani, nyoka ya kale, ilijiingiza kati yetu kupitia karama ya unabii. Masemi: „Hivi asema BWANA mtumishi wangu…“ inageuka“ Hii asema mwana mke“. Mwito na yale ambayo BWANA ali mwambia mtumishi

wake siku, Aprili, 2, 1962, yalitiliwa mashaka kile kilichofanyika katika bustani ya Edeni kilifanyika tena mahali hapa: „Kweli BWANA aliongea naye…?“ Nikwa namna hiyo mahali hapa kulioneka mbegu ya aina mbili, kama vile Kaini na Abeli.

Kupitia uovu na mabishano chini ya ushawishi wa nyoka, alisambaza sana: „BWANA hakuongea naye“. Kanisa la mahali ili bomolewa. Waamini wa ujumbe wa wakati wa mwisho ulimwenguni pote wamezoeleshwa kuingizwa katika upotevu.

Nani awezae kuielewa? siku Juni, 6, 1979 BWANA Mungu alitoa sauti kubwa kama vile ngurumo zina vyo toa sauti yake, yale maneno tisa mamoja aliyosema katika bustani ya Edeni myaka elfu sita inaisha: *„Kwa kuwa umesikiliza sauti ya mwanamke“*. Mapenzi yasiyo makamilifu ya Mungu hapo ingeweza kutimia, ilikwa sasa iweze mapenzi makamilifu ya Mungu katika waamini wa kweli; na mbegu ya kweli.

Yale yaliyo tendeka mbinguni na katika bustani ya Edeni yako nyuma mbali nasi. Lakini yale yaliyo tendeka katikati yetu yame tuletea huzuni kubwa. Mbegu mbili tofauti za kiroho zilionekana: wamoja waamini utume wa kimungu wengini wana beuwa na kuchekelea. Wale wote wanaokuwa chini ya ushawishi mbaya, hawa jaweka mguu yao katika maskani, hapa kwenye kituo cha Misheni tangu Mai, 1979 hadi sasa.

Na hata sasa ni kuhusu mbegu mbili: kwa wamoja wanaamini kwamba BWANA mwenyewe alitoa utume wa Kimungu katika mupango wa okuvu kupitia mwito wa hapo hapo, ambayo imetumika ulimwenguni, muda wa nusu karne. Wengine wanadumu katika mafundisho inayo shuhudia kwamba ndugu Branham ndie mutangulizi wa kuja kwa pili kwa Kristo, eti siyo Ujumbe na wanamgojea aweze kurudi na kumaliza kazi yake katika hema.

Hudma yake ya kipekee niliyo shuhudia mimi mwenyewe ilikuwa sawa sawa na ile iliyo tendeka katika hudma ya BWANA wetu. Ndugu Branham alirudilia akiweka mkazo, akilinganisha hili na mwanzo 18, inayo onyesha mazungumuzo ambayo Mungu alikuwa nayo pamoja na Ibrahim, na Yn 5:19. Lakini sasa, na anaendelea kutukuzwa kupitia mafundisho ya uongo, inayo wangoza kwa kuabudu sanamu kunayo fanyika karibu naye. Wanapita pembeni kwa yale ambao Mungu anayo yafanya kwa sasa, kupitia

kukataa Yule anae chukuwa ujumbe wa Neno: kwa kufanya hivyo, wanamfanya BWANA mwenyewe kuwa muongo pia nabii alie ishuhudia. Mungu anawaambiya: *"Tazameni, enyi mnaodharau, kastaajabuni, mkatoweke; kwa kuwa natenda kazi mimi siku zenu kazi ambayo msinge isadiki kabisa, ijapo mtu akiwasimulia sana"* (Matendo 13:41).

Katika wa Efes 6; tunaambiwa: *"Vaeni silaha zote za Mungu mpate kuweza kuzipinga hila za shetani; kwa maana kushinda na kwetu sisi si juu ya damu na nyama bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa Roho"* (Shahiri 11-12).

Kila shahiri ya sura hii inamo kitu cha muhimu ambacho tunastahili kusikiliza na kuheshimu.

"Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, ***na upanga waroho ambao ni Neno la Mungu..."*** (Shahiri 17) Mutume aliilinganisha ku neno la Mungu kama **"Upanga wa kiroho"** katika muktadha wa vita vya Kiroho. Aliwaita waamini waje kwa kuombeana moja kwa mwengine nayepia aliomba kuombewa kwa shahiri ya 19***: „Pia na kwa ajili yangu mimi nipewe usemikwa kufumbua kinywa changu, ili niihubiri kwa ujasiri ile siri ya injili..."***

Katika Ufun 12:10-11 tuna soma kuhusu wale waliyo shinda na wana semu kwa unyakuo: ***"Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, sasa kume kuwa wokovu, nanguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa Ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku. Nao wakamshinda kwa damu ya mwana kondoo, na kwa neno la Ushuhuda wao; ambao hawa kupenda maisha yao hata kufa."***

Neema ya Mungu

Kwa furaha kubwa twaweza shukuru Mungu kwa neema yake. Tusipo jail na kusingiziwa na kuzihakiwa na hata vitendo vya mauwaji ya kitabia iliyo anza tangu mwaka wa 1979. Lakini BWANA Mungu alitujalia neema. Si kwa Kanisa la mahali pekee, baali na katika kazi ya umishonari ulimwenguni pote. Kati ya 200 na 300 ya wandugu na wa dada, kutoka mkoa yote wanashiriki

mikutano ya juma ya mara kwa mara. Kwa wikendi ya kwanza ya juma ya kila mwezi, kuna fika waamini 1200 kutoka Ulaya nzima na mainchi tofauti za dunia, wanao kuja kusikiliza neno la Mungu. Mikutano inayo tufuata kwenye mtandao, kwa mikutano yetu ya wikendi ya kwanza ya kila mwezi imeongezeka mpaka kufikia inchi 172 kwa mwezi huu wa karibu.

Hudma ya ajaabu ya Ndugu Branham ilifikia ukomo wake kwa mwaka 1965. Kiisha kukaja nyakati za Baraka kati ya myaka 1966 na 1979 na sasa tunapotazama nyuma myaka 40 imepita, tunaona namna Mungu alivyo kuwa pamoja nasi kwa namna yote kupita kipimo.

Unajua namna gani Ndugu Branham alivyo iacha Biblia yake ikiwekwa nyumbani? ilibaki ikifunguliwa kwenye meza ya Ofisi yake, kwa sura ya mwisho ya kitabu cha kumbukumbu la torati, sura ya 34, na kwa mwanzo wa kitabu cha Yoshua, sura 1. Chini ya uongozi wa Musa kutoka utumwani huko misri, na kupitia uongozi wa Yoshua waliingia kwenye Inchi ya ahadi. Kwa kupitia hudma ya Ndugu Branham hapo kulianza mwito wa kutoka katika utumwa wa kidhehebu na sasa, tunaishi katika kuingia kwa Mungu katika maahadi zote.

Wakati Ndugu Branham alipo ongea kuhusu muhuri wa saba aliomba hivi kwa dakika za mwisho**: "Sasa, BWANA ninaomba unisaidie ninaanza pungukiwa kidogo, kidogo, BWANA. Nina jua kwamba siku zangu sinyingi tena, natena na kuomba unisaidie, niwe mwaminifu na wa kweli na mwenye haki, ili niweze kuchukua ujumbe mbali kama vile ulivyo ni kubalia kuichukuwa. Na itakapo kuja watika wangu wa kupumuzika, ambao nitakapo shuka kwenye mtoni, na mawimbi yatakapo anza kuja kunichukua, Ee Mungu ni weze kuipokeza upanga huu kwa mtu mwengine, ambae atakuwa mwaminifu kwa hii, BWANA, na aichukue kweli."**

Naweza nikaulize, ni nani basi alie kuwa wa kwanza kuuchukuwa Ujumbe katika ulaya wa kaskazini na ulaya wa kusini, katika Azia na Afrika na katika ulimwengu pote?. Kuna mwengine duniani ambaye alie wai kuisikia sauti ya BWANA, na kupokea mwito wa Kimungu na kufanya kazi ya Utume kama vile sehemu

ya mpango wa Okovu? Wote walio wa Mungu wa nasikia maneno ya Mungu (Yn 8:47) na walitambuwa kwamba kuna ujumbe wa mwisho, wa mwito wakutoka, na kurudishwa, na kujitenga, na matayarisho. Mbele ya kurudi kwa karibu sana kwa Kristo, wote wanao amini kwamba kutumwa kwa hapohapo, kunafungwa kwa mpango wa wokovu wa Mungu wana jitahidi sasa na wana macho yenye kubarikiwa kwa kuwa wanaona, na wana masikio yenye kubarikiwa, kwakuwa yana sikia (Lk 10:23) na watapata sehemu kwa unyakuo kama wabarikiwa wa BWANA.

Ndugu Branham hakuuchukua ujumbe kwa inchi nyingine. Baada ya kufunuliwa kwa mihuri saba kwa Machi 1963, hata hakuhubiri inje ya inchi yake. Kwa sasa naweza kutazama nyuma kwa myaka nyingi ambamo nime hubiri ujumbe wa kibiblia wa kipekee kupitia utume wa Kimungu wa hapohapo katika inch 165, kwa miji mingi ulimwenguni, na huko Moscow, Beijing, Cairo, na Damascus. Na tukiongeza utangazaji wa ki televisheni, nime hubiri mahuri zaidi ya elfu kumi na moja. Kwa wakati huu, mahubiri yaliyo kamatwa kwa ajali ya mpango wa kitelevisheni, yanaendelea sambazwa katika inch 72, kufwatana na mahali tofauti, wanao tufuata ni idadi ya million 10 ao 12.

BWANA Mungu amenijalia neema kubwa ya kuweza kutafsiri mahubiri ya Ndugu Branham pia na kuandika Vitabu, na ma Brosha, na Mabaruwa za mzunguko. Nilijaribu kukomboa muda na ni mekwisha safiri safari za angani kilomita Millioni 24 za kimishonari za kila mwezi. Kuna jambo moja linalo nihuzunisha kwa kilindi cha moyo wangu: ni kwamba tangu mwaka wa 1979, kundi nyingi zinazo jiita makanisa za ujumbe zimejitokeza katika miji mingi. Kulingana na Biblia, kuna stahili kuwa tu Kanisa Moja la Mungu anaye ishi katika kila muji. Mengine yote ni Makundi zilizo undwa na watu zina ishi chini ya ushawishi wa wanadamu wanao tangaza matafsiri yao waki jilinganisha na nabii. Paulo alitoa arifa*: "Ndugu zangu, na wasihi, waangalieni* ***wale wafanyao fitina na mambo yakukwaza kinyume cha mafundisho mulio jifunza; mkajiepushe nao." (***Rom. 16:17)

Mungu mwenyewe aliweka hudma katika Kanisa (Efes 4:11, 1Kor 12:28). Yeye mwenyewe ndie aliye weka utume wa mwisho. Wandugu wote walio geuka kutoka kwenye ukweli wana fwata

njia zao wenyewe na wanakataa Neno. Wote wanajilinganisha kwenye nukuu na kwa njia hiyo wana unda makundi hizo. Kwangu mimi, yaliyo andikwa yanadumu kuwa kweli***: "Maana hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu zake BWANA wetu Yesu Kristo na kuja kwake; Baali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake … Nasi tuna lile Neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo mkiliangalia, kama taa ingaayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu…"*** (2. Pet 1:16-19)

Tangu myaka hii yote sija wayi kuigiya kwenye mabishano za manukuu yoyote, lakini nilihubiri neno pekee. Tuna soma na kusikiliza mahubiri na tunayaacha ginsi yalivyo. Sifa zimurudilie BWANA mwaminifu, kwa kuwa naweza tegemea neni la 2 Tim 4:17: ***"Lakini BWANA alisimama pamoja nami akanitia nguvu, ili kwa kazi yangu ule ujumbe utangazwe kwa uvumilifu, hata wa sikie mataifa yote; nami nikaokolewa katika kinywa cha simba."***

Katika ulimwengu nzima; tunagabulia wateule wanao amini maahadi za Mungu na chakula cha kiroho cha wakati huu. BWANA alisema wazi mambo yafwatayo kuhusu wale aliyo watuma: *"Awasikilizae ninyi anisikiliza mimi, naye awakataaye ninyi anikataa mimi; naye anikataaye mimi amkataa yeye aliye nituma."* (Lk 10:16) Amina. Ni hivyo ilivyo.

Twaweza kuona Mt 24:14 ikitimilika machoni petu: ***"Tena habari njema ya Ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapo kuja."***

Mataifa yote – Hii siyo ya kawaida. Ni lazima injili ya kimusingi ya milele*: "Kisha nikaona Malaika mwingine akiruka katikati ya mbingu mwenye* ***injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi na kila taifa na kabila na lugha na jamaa…"*** (Ufun 14:6)

Upendo kamili Ndio Utakao Ingia Huko

Sikilizeni enyi waamini wa mataifa yote na kabila zote: Bwana arusi alie neno ye mwenyewe atachukua bibi arusi neno pekee! Huko mbinguni kutakuwa bibi arusi alie oshwa katika damu ya mwana kondoo, alie takaswa katika neno la kweli, naku wekwa muhuri wa Roho mtakatifu. Sasa kilamutu amepewa bahati ya mwisho ya kuchaguwa kama atakuwa kwa upande wa mabikiri wenye Busara ao kwa upende wa mabikira wapumbafu. Neno la wakati wetu lime kuja kutoka kwa Mungu. Nalitatimiza kile ambachi Mungu amelituma kufanya***: "Ndivyo litakavyo kuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu, halita ni rundia bure, baali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale nililo lituma"*** (Isa 55:11). Amina. Amina.

Manabii wote, na mitume wote, na wale wote waliyo tumwa walitimiza utume wao. Ndugu Branham aliyafanya yale ambayo ali amriwa kufanya, nami niliyafanya yale ambayo BWANA mwaminifu aliyo ni agiza kufanya. Bibi arusi anarudi kwa hatua, kama vile Ndugu Branham alivyo sema siku, Julai, 5, 1964: **"... kwa ujao wa mustari wa Neno".**

Nitamaliza mwaka wa 85 wa maisha yangu kwa Disemba 2018. Nyakati za safari za mwezi zina anza ku punguka; Kutembea, Kuona, Kusikia. Lakini neno lililo andikwa kwenye moyo lina dumu. Ashukuriwe Mungu kuona makanisa, namakundi za nyumbani zote ulimwengini pote, zina weza kusikia, na kuona na kuishi yale ambayo Mungu anafanya kwa sasa.

Nikutoka kilindi cha moyo wangu, nina shukuru kila mmoja wenu duniani pote kwa ajili ya maombi yenu. Mungu mwaminifu awabariki nyote, aimarishe imani ya milele na iwe uhakika katika maisha yenu. Kama vile munavyo amini ujumbe wa kibiblia, na hivyo ndivyo mutakavyo ishi utimilifu na kuwa na sehemu katika unyakuo. Nashukuru BWANA wangu ambae alie nionesha ono kubwa la unyakuo kwa Januari, 1981, ndiyo tutanya kuliwa sote pamoja: ***"Kwa maana BWANA atatimiza kazi yake duniani, bila kukawia."*** (Rom 9:28)

Mume sikiya ya kwamba Ndugu Helmut Miskys amechukuliwa kwenye utukufu. Nataka ni wajulishe kwamba huyu mpendwa

wetu ame barikiwa sana na BWANA alimtumikisha kwa namna ya ajabu, iwe katika familia yake ao katika familia za watoto wake, hata kwa kanisa la mahali ao alipo ongoza shule la jumapili, hata kwa mikutano ya vijana, hata kwa inchi zenye lugha ya kiportigali: aliacha njia za Baraka mahali pote. Tunaomba pole na mibaraka ziweze kuwafikia familia ya Ndugu Helmut Miskys, na dada Erika Miskys. Ndugu Claudio miskys alishika uongozi wa kiroho na kushugulikia waamini katika Brasilia na katika inchi nyingine zinazo ongea lugha ya kiportigali. Tunashukuru Mungu kwa kuona ameshughulikia mambo yote na kutayarishia taifa lake.

Picha hii tulipata kutoka kwa Dada Erika Miskys, inayo onesha Ndugu Helmut Miskys akiwa Havana huko Cuba wakati wa safari yake ya kimishonari kwa Machi, 2018.

Kwa mwisho wa mwaka na kwa mwaka ujao, tuna watakia nyinyi nyote mibaraka ya ajabu ya mwenye nguvu zote. Na hii iweze kuwa mwaka wa Yubili (Law 25:8-13, Lk 4:16-21). Mungu mwaminifu na awabariki nyote katika mataifa yote na katika lugha zote. Nikumbukeni katika maombi yenu. Aksanti sana.

Kwa utume wake,

Bro. Frank

Ikiwa unapendezwa kupokea vitabu vyetu,
waweza kutuandikia kupitia anwani ifwatayo:

Kituo cha Misheni
Sanduku la Posta 100707
47707 Krefeld
Ujerumani

Waweza kuingia kwenye mtandao wakati wa mikutano yetu ya wikendi ya kwanza ya mwezi. Siku ya Jumamosi Jioni pa saa 19:30 h (Saa ya kati ya Ulaya), Jumapili asubuhi pa saa 10:00 h. Mikutano ya weza kusikilikana katika Lugha 13 tofauti duniani pote.

Pokeeni sehemu kwa yale ambayo Mungu anayo yafanya sasa kulingana na mpango wake wa okovu!

Ukurasa wa vuti: http://www. freie-volksmission. de

Barua pepe: volksmission@gmx. de

Fax: +49-2151/951293

Na mwandishi na mchapishaji E. Frank